**Journal of Kiswahili and Other African Languages**
Vol. 1 No. 1 (2023): ISSN (Online): 2958-4914
DOI: https://doi.org/10.58721/jkal.v1i1.96


# Ulinganishi wa Msamiati baina ya Kikamba, Kigweno na Chasu: Tathmini ya Nadhariatete ya Ndugu na Ndugu wa Mbali

**Fatuma Abadalah[1], Sarah Ndanu M. Ngesu[2] & George Yesse Mrikaria[3]**
[1]Baraza la Kiswahili la Taifa (BAKITA)
[2]Chuo Kikuu cha South Eastern Kenya
[3]Chuo Kikuu cha Dar es Salaam

**Uwasilishaji wa Makala**
*Pokelewa: 2023-03-28*
*Rekebishwa: 2023-04-17*
*Kubalika: 2023-05-16*
*Chapishwa: 2023-05-20*

***Maneno Muhimu***
Isimu
Kibantu
Kigweno
Kipare
Kikamba
Ulinganishaji

**Jinsi ya Kurejelea Makala:**
Fatuma A., Ndanu, S. M., Ngesu, N. S. M., & Mrikaria, G. Y. (2023). Ulinganishi wa Msamiati baina ya Kikamba, Kigweno na Chasu: Tathmini ya Nadhariatete ya Ndugu na Ndugu wa Mbali. *Journal of Kiswahili and Other African Languages*, *1*(1), 47-69.

*Copyright © 2023*
CC BY NC SA

**Ikisiri**
Makala haya yanachunguza kiulinganishaji msamiati wa lugha tatu za Kibantu, mbili zinazungumzwa nchini Tanzania na lahaja mbili za Kikamba zinazozungumzwa nchini Kenya. Lengo la Makala haya ni kutathmini maoni ya Massamba (2017) kuhusu nadhariatete ya ndugu na ndugu wa mbali. Lugha zinazotambuliwa kuwa 'ndugu' ni zile zilizo katika mtagusano wa karibu na zile zinazojulikana kama 'ndugu wa mbali' ni lugha zinazotokana na fuko hilo moja lakini zilizo mbali kimasafa. Data iliyotumiwa katika makala haya ilikusanywa uwandani kupitia orodha ya msamiati wa msingi uliopewa wazungumzaji wa Kigweno, Kipare na lahaja mbili za Kikamba. Vilevile data hii imetajirishwa na uzoevu wa waandishi kama wazungumzaji wazawa wa lugha zinazojadiliwa. Katika kujaribu kuthibitisha "Udungu" wa lugha hizi tulitumia kigezo muhimu cha kiisimu cha Mbinu Linganishi ambayo hutumika kulinganisha lugha mbalimbali kwa lengo la kuonesha kama lugha hizo zinatoka katika fuko moja au zinatokana na mafuko ya lugha tofauti. Ingawa katika mbinu linganishi kuna mambo kadha yanayochunguzwa, tumejikita kuchunguza na kuchanganua msamiati wa msingi, mfumo wa maumbo ya maneno, maumbo ya sauti na mfumo wa uainishaji wa nomino katika lugha zinazohusika. Makala haya yamebaini kwamba kuna ulinganifu wa kiwango kikubwa, baina ya lugha za Kikamba, Kigweno na Chasu ingawa wazungumzaji wake wako katika nchi tofauti (Kikamba-Kenya, Kigweno na Chasu-Tanzania) na hawana utangamano wa kila siku. Kufanana huko

kumebainika katika msamiati wa viunngo vya mwili kwa 52 %, msamiati wa mazingira asili kwa 59% na msamiati wa matendo ya kila siku kwa 65 %. Pia, imebainika kuna kutofautiana kwa msamiati wa viunngo vya mwili kwa 48 %, msamiati wa mazingira asili kwa 41 % na msamiati wa matendo ya kila siku kwa 35%. Msamiati mwingi unashabihiana kwa sauti na panapotokea tofauti ya sauti imebainika sauti hizo zinatamkiwa mahali pamoja au zimetokana na kuathiriwa na lugha jirani na pia kutokana utengano wa muda mrefu. Hivyo, lugha za Kikamba, Kigweno na Chasu zina mnasaba wa karibu jambo linalodhihirishwa na msamiati wa msingi pamoja na mfumo wa sauti. Aidha, wazungumzaji wa Kigweno na Chasu wanatangamana mara kwa mara nchini Tanzania na hivyo kama ilivyo Nadhariatete ya Ndugu na Ndugu wa Mbali kuna kufanana kwa msamiati kuliko lugha hizo zinavyofanana na Kikamba. Aidha, ilibainika kwamba kinyume na inavyodaiwa na Nadhariatete kwamba Ndugu wa Mbali watatofautiana kwa kiasi kikubwa, lahaja ya Kikamba ya Mwingi inayozungumzwa mbali sana, Kaskazini mwa Kaunti ya Kitui inashabihiana kisauti na lugha ya Chasu nchini Tanzania tofauti na lahaja ya Kikamba ya kimaandishi.

## Utangulizi

Sura hii inalinganisha msamiati wa lugha tatu za Kibantu ambapo lugha mbili zinazungumzwa nchini Tanzania na lahaja mbili za Kikamba zinazozungumzwa nchini Kenya. Lengo la sura hii ni kutathmini maoni ya Massamba (2017) kuhusu Nadharia tete ya Ndugu na Ndugu wa Mbali. Massamba anaeleza kwamba jamiilugha mbili ambazo zina uhusiano mnasaba, yaani zinatokana na mame-lugha moja na zipo katika mtagusano wa kijamii, kiuchumi au kisiasa huathiriana zaidi kuliko lugha za aina hiyo hiyo ambazo ziko mbali zaidi kimasafa. Lugha zinazotambuliwa kuwa 'ndugu' ni zile zilizo katika mtagusano wa karibu na zile zinazojulikana kama 'ndugu wa mbali' ni lugha zinazotokana na fuko hilo moja lakini zilizo mbali kimasafa. Katika kujaribu kuthibitisha "Undugu" wa lugha hizi, tulitumia kigezo muhimu cha kiisimu cha mbinu linganishi. Kwa mujibu wa Massamba (2017), mbinu linganishi hutumiwa na wanaisimu kujaribu kulinganisha lugha mbalimbali kwa lengo la kuonesha kama lugha hizo zinatoka katika fuko moja au zinatokana na mafuko ya lugha tofautitofauti. Ingawa katika mbinu linganishi kuna mambo kadhaa yanayochunguzwa, tumejikita kuchunguza na kuchanganua msamiati wa msingi wa lugha hizo tatu.

## Lugha ya Kikamba

Kikamba ni lugha inayozungumzwa na watu waitwao Wakamba ila wao wenyewe hujiita Akamba. Wakamba huishi katika kaunti za Kitui, Machakos na Makueni, Mashariki mwa nchi ya Kenya. Mollig na Heinne (1980) kama wanavyonukuliwa na Ngesu (2004) waliainisha wazungumzaji wa Kibantu katika makundi matano. Kikamba ni miongoni mwa lugha za Kibantu za Tawi Kuu la Lugha za

Kibantu[1]. Guthrie (1967) aliwaweka Wakamba katika kundi la 50 katika kanda E. Lugha katika kundi hili ni kama zifuatavyo: Kikuyu (E51), Kiembu (E52), Kimeru (E53), Kitharaka (E54), Kikamba (E55) na Kithaisu (E56). Lugha hii huainishwa katika kundi moja na lugha kama vile Kikuyu, Kimeru. Kitharaka, Kiembu na Kimbeere.

Neno 'Kikamba' linalorejelea lugha yenyewe limeundwa kwa mofu [ki] ambayo ni kiambishi na mofu

[-kamba] ambayo ni mzizi.

Kuhusu mzizi 'kamba', Mathooko (2004) na Ngesu (2004) wanasema kwamba mzizi huu haujafaulu kupata maana ya kisemantiki lakini mzizi wenyewe unapopachikwa viambishi huleta maana zifuatazo:
Mzizi 'kamba' unapowekwa kiambishi awali [u] na kiambishi tamati [ni] tunapata neno u-kamba-ni kwa maana ya eneo la asili la Wakamba.
Mzizi 'kamba' ukipachikwa kiambishi awali [u] pekee tunapata neno 'u-kamba[2]' linalomaanisha eneo wanapopatikana Wakamba.

Mzizi 'Kamba' ukiongezwa kiambishi awali [mu] huunda neno 'mu-kamba' lenye maana ya umoja wa 'Akamba' kama wanavyojitambulisha wenyewe. Katika maandishi yanayohusu Kikamba, neno "kamba" limetumika kwa maana ya watu na pia lugha. Tunataka kusisitiza kwamba neno hili ni mzizi tu ambao unahitaji kupachikwa viambishi mwafaka kulingana na muktadha wa matumizi ili kuleta maana yake kisemantiki. Katika muktadha wa lugha ya Kiswahili, tunaweza kupata maneno 'Mkamba' (umoja), 'Wakamba' (wingi) na 'Ukambani' (eneo linalomilikiwa na Wakamba).

**Historia Fupi Kuhusu Jamii ya Wakamba**
Kuna simulizi za kihistoria zinazotolewa na jamii ya Wakamba kuhusu asili yao. Mojawapo ya simulizi hizi inarejelewa katika kazi za watafiti kama vile Mutiga (2002), Mathooko (2004) na Ngesu (2004) kwamba Wakamba walitoka Congo wakiwa miongoni mwa Wabantu wengine. Walifika 'Kiima Kyeu' kwa maana ya 'Mlima Mweupe' yaani Kilimanjaro, na kufanya sehemu hiyo kuwa makazi yao. Baadaye Wakamba walitoka eneo hilo na kuhamia sehemu ya Kyulu ambayo wakati huo ilikuwa sehemu ya mkoa wa Machakos ila kwa sasa ni sehemu ya kaunti ya Makueni.

Kabla ya kuanza safari kuelekea Kyulu kutoka Kiima Kyeu (Kilimajaro), kulizuka ubishi miongoni mwao. Walikuwa hawakubaliani kuhusu njia watakayofuata, ndipo ulipozuka usemi kuwa 'ĩnywĩ yu mwĩamba ata?'ko mwĩ andu ma kûamba tu?' kwa maana ya 'sasa nyinyi mnasema nini ('mnaambaje')? 'Kwani nyinyi ni watu wa kusemasema tu? Kwa hivyo, kwa mujibu wa simulizi hii, huo ukawa mwanzo wa neno Wakamba (watu wa kuamba/watu wa kusemasema). Hata hivyo, kuna madai mengine ya kimapokezi kuwwa jina hili linatokana na mti ujulikanao kwa lugha ya Kikamba

[1] Tawi kuu la Lugha za Kibantu ni tafsiri ya *Central Branch of Bantu Languages*.

[2] "Ukamba" ni kama wananavyotumia wao wenyewe Wakamba na kwa Kiswahili linatumika neno "ukambani"

'Mûamba' yaani mbuyu ambao hupatikana kwa wingi ukambani hususan sehemu za nyikani (Ngesu, 2004).

Simulizi nyingine ya kimapokeo inayofanana kwa kiasi na inayorejelewa na watafiti tuliowataja hapo awali ni ile iliyoandikwa kwa mara ya kwanza na Mmisionari Ludwig Krapf (1849). Kulingana na simulizi hii, Wakamba walitokea Kusini mwa Kenya katika eneo la Mlima Kilimanjaro. Kwa mujibu wa simulizi hii, Wakamba walihama kutoka eneo la Mlima Kilimanjaro wakitafuta maji kutokana na makali ya ukame wa miaka mingi. Wataalamu wengi wanaonekana kukubaliana na maoni haya kwa sababu hakuna marejeleo yoyote yanayoonesha migogoro au vita baina ya Wakamba na jirani zao ambayo ingewasukuma kuhama.

Simulizi hii inaendelea kueleza kwamba, mwanzoni Wakamba walikuwa wafugaji na walimiliki mifugo wengi hususani ng'ombe na mbuzi sawa na Wamasai. Hata hivyo, tofauti na Wamasai ambao walitegemea mifugo kwa maisha yao ya kila siku, Wakamba walijishughulisha na ukulima, ukusanyaji wa matunda na mizizi inayofaa kuwa chakula pamoja na uwindaji. Walipohamia katika eneo la Ukambani hususan Milima ya Mbooni, walishawishika kuendeleza kilimo kutokana na hali ya eneo hilo lililokuwa na rutuba na mvua nyingi. Hali hii iliwachochea kukaa hapo na kuendelea kusambaa katika eneo lote ambalo kwa sasa linajulikana kama Ukambani.

Simulizi nyingine ya kimapokeo imerekodiwa na Laurie (2007). Kwa mujibu wa mtaalamu huyu, simulizi hii inategemea makundi tofauti ya Wakamba. Laurie amewagawa Wakamba katika makundi manne kama ifuatavyo:

1. Wakamba wa Ûlû ama Ĩveti (ûlû ina maana ya mahali palipoinuka/juu)
2. Wakamba wa Kibwezi au Kĩkûmbûlĩu
3. Wakamba wa Kĩtui
4. Wakamba wa Muumonĩ.

Kulingana na simulizi hii iliyorekodiwa na Laurie (2007), Wakamba wa Ûlû wanadai asili yao ni Kusini mwa Kilimanjaro. Simulizi za kimapokeo kwa mujibu wa Wakamba wa Muumonĩ zinasema wao wanaamini walitoka karibu na eneo la Wagiriama, pwani ya Kenya. Halikadhalika, wanadai wazee wao wa kwanza walitoka eneo hilo karibu na Wagiriama kwa kupiga mbizi huku wakitumia mizinga ya nyuki na kuvuka mto Athi hadi kufikia eneo pana la Kaskazini ya Kaunti ya Kitui, nchini Kenya. Kwa mujibu wa historia na baadhi ya simulizi za kimapokeo, mwanzoni Wakamba walikuwa wawindaji hodari wa ndovu kwa minajili ya kupata pembe ili kushiriki katika biashara baina yao na Waarabu. Walibadilishana pembe za ndovu na kupewa shanga na nguo. Katika karne ya 19, Wakamba walishiriki katika misafara ya biashara kutoka bara hadi pwani. Katika miaka ya 1850 na 1960 pamoja na jamii ya Miji-kenda, Wakamba walisaidia kusafirisha bidhaa kutoka Mombasa hadi Lamu. Hii ni njia mojawapo iliyochangia kuhama kwa baadhi yao kutoka eneo la Ukambani na kusambaa mahali kwingineko nchini Kenya na Tanzania.

Mulatya (2013) anaeleza kwamba Wakamba waliingia Kenya wakitokea Tanganyika, Kaskazini mwa Tanga. Kutoka katika eneo hilo, walitembea kupitia Milima ya Taita na kufika eneo linalojulikana kwa sasa kama Kaunti ya Machakos. Mulatya anaendelea kuelezea kwamba kutoka eneo hilo la Machakos,

Wakamba walisambaa katika maeneo mengine ya Ukambani kama vile Kitui. Simulizi za kihistoria zinaeleza kwamba wale walioelekea Kitui walikuwa wafugaji wa ng'ombe.


Muthoka (2017) akiwanukuu Lewis, Gray na Charles (2013) anaeleza kwamba Wakamba walihamia Kenya kutoka Magharibi mwa Tanzania katika eneo linalojulikana kama Unyamwezi karibu na Milima ya Usambara.

Kwa kurejelea maelezo hayo yanayotolewa na watafiti, inabainika kuwa wanakubaliana kwamba Wakamba waliingia Kenya kutokea Kaskazini mwa Tanzania, eneo la Mlima Kilimanjaro.

**Lahaja za Kikamba**

Watafiti mbalimbali wameainisha lahaja za Kikamba katika makundi tofautitofauti. Maundu (1980) aliainisha lahaja za Kikamba katika makundi manne kwa kuonesha lahaja mbili kuu ambazo kila moja ina lahaja ndogo mbili ndani yake. Kwa mujibu wa Maundu, lahaja kuu za Kikamba ni Kĩmasakû na KĩKĩtui. Majina ya lahaja hizi yanatokana na jina la eneo. Lahaja ya Kĩmasakû ina lahaja mbili, moja huzunguzwa katika Kaunti ya Makueni na nyingine katika Kaunti ya Machakos. Lahaja ya KĩKĩtui ina lahaja mbili, moja huzungumzwa eneo la kaunti ndogo ya Mwingi na ile nyingine katika maeneo yale mengine ya kaunti ya Kĩtui. Tunataka kusisitiza kwamba hata kama maelezo anayotoa Maundu (1980) yana mashiko kiasi, utafiti wake ulifanywa miaka mingi iliyopita na lugha haituami bali hubadilika kulingana na wakati. Pia, watafiti waliofuata walitambua kwamba Kimasaku kina lahaja nyingi na wala si mbili kama anavyoeleza Maundu. Halikadhalika, lahaja ya KĩKĩtui ina lahaja nyingi kuzidi alizoelezea Maundu kama inavyooneshwa katika Kielelezo Na. 1.

**Kielelezo Na. 1: Lahaja za Lahaja Kuu ya KĩKĩtui**




Mutiga (2002) hakujishughulisha na uainishaji wa lahaja za Kikamba bali alichunguza tofauti zinazotokana na toni baina ya lahaja mbili kuu za Kikamba yaani Kĩkĩtui na Kĩmasakû. Mutiga anaeleza kwamba pale lahaja ya Kĩmasakû inapotumia toni ya juu, mara nyingi lahaja ya Kĩkĩtui hutumia toni ya juu. Hata hivyo, utafiti wa Mutiga ulijikita katika mojawapo wa lahaja ndogondogo za lahaja ya Kitui inayozungumzwa Kaskazini mwa kaunti ya Kitui hususani katika kaunti ndogo ya Mwingi. Mutiga (2002) anaeleza kuwa lahaja inayozungumzwa katika kaunti ndogo ya Mwingi hutofautiana na lahaja nyingine za Kikamba kitoni, kisauti na kilekisika.

Maundu (1980), Mutiga (2002), Ngesu (2004), Mulatya (2013) na Muthoka (2017) wanatambua lahaja tano za Kikamba ambazo zimetokana na lahaja kuu mbili yaani KĩKĩtui na Kĩmasakû. Lahaja hizi ni:

1. KĩKĩtui inayozungumzwa katika kaunti ndogo ya Mwingi na viunga vyake.
2. Lahaja ya Kitui kati inayozungumzwa sehemu za Kitui kati na sehemu nyinginezo.
3. Lahaja ya eneo la Mashariki na Kusini mwa kaunti ya Kitui inayodhihirisha tofauti za kilafudhi.
4. Lahaja ya Kĩkĩlûngû inayozungumzwa eneo la Kĩkĩlûngû na viunga vyake.
5. Lahaja ya Machakos (Masakû) inayotambuliwa na watafiti wengi kama lahaja mojawapo kuu ya Kikamba yaani Kĩmasakû.

Kama anavyoeleza Ngesu (2004), lahaja inayozungumzwa eneo la Kaskazini mwa kaunti ya Kitui inayojulikana inatofautiana na lahaja nyingine za Kikamba kwa kuwa na sauti [r] na [gh] ambayo hunukuliwa kifonolojia kama [ɣ] ambazo hazipo katika othografia ya Kikamba. Hata hivyo, makala hii imebaini kwamba sauti hizi zipo katika Kigweno, Chasu1 na Chasu 2.

**Lugha ya Kigweno**

Kigweno ni lugha inayozungumzwa katika eneo la Ugweno katika wilaya ya Mwanga, mkoani Kilimanjaro, nchini Tanzania. Eneo hili limepakana na wilaya ya Taita Taveta (Kenya) kwa upande wa Mashariki, wilaya ya Moshi Vijijini na wilaya ya Rombo kwa upande wa Kaskazini, tarafa ya Usangi kwa upande wa Magharibi na tarafa ya Butu kwa upande wa Kusini (taz. Sewangi, 2008). Kigweno ni mojawapo ya lugha zilizoainishwa na Guthrie (1967) katika kundi E.65. Guthrie katika uainishaji wake anaiweka lugha hii pamoja na nyingine za lahaja ya Kichaga zinazoongelewa katika maeneo ya Mlima Kilimanjaro. Lahaja hizo ni: kundi E.62a, b, na c, Rwo E.61 inayozungumzwa katika miteremko ya Mlima Meru na Kahe E.64 inayozungumzwa katika bonde la Mlima Kilimanjaro karibu na Mji wa Kahe. Kutokana na uainishaji wa Guthrie lugha hizo zina uhusiano wa karibu sana. Mtazamo huu unaoichukulia lugha ya Kigweno kama lahaja ya Kichaga unaungwa mkono pia na wataalamu kama vile Nurse na Philippson (1980) na Winter (1980) (taz. Philippson, 2000).

Mtazamo wa Philipson (2000) kuhusu lugha ya Kigweno ni tofauti na wa Kimambo (1969); Nurse na Philippson (1980) na Winter (1980) wanaamini kwamba Kigweno ni lahaja ya Kichaga. Philipson (2000) anaeleza kwamba inashangaza Kigweno kuwa lahaja ya Kichaga ilhali kwa muda mrefu lugha hii imetenganishwa na lugha nyingine za Kichaga zinazozungumzwa katika mteremko wa Mlima Kilimanjaro na kwamba lugha hii imeathiriwa kwa kiasi kikubwa na lugha ya Kiswahili na Chasu. Maelezo ya Philipson yanaonesha kwamba lugha ya Kigweno haiwezi kufanana na lugha za Kichaga kutokana na Kigweno kujitenga na lugha hizo kwa muda mrefu lakini pia kwa kuwa lugha ya Kigweno imeathiriwa na lugha ya Chasu na Kiswahili. Akishadidia kuhusu Kigweno kuathiriwa na Chasu Philippson (2000) anaeleza kwamba ingawa asili ya lugha ya Kigweno na lugha nyingine za Kichaga ni moja, Kigweno kimeathiriwa zaidi na lugha ya Chasu. Anaongezea kwamba kutokana na athari hizo, Wagweno wa sasa hivi wanazungumza Chasu sambamba na lugha yao wenyewe. Anaeleza pia kwamba kwa sasa Wagweno wengi wanaongea Kiswahili.

Naye, Mreta (2000) akimuunga mkono Philipson (2000) anaeleza kwamba kwa kuchunguza kipengele cha msamiati, inaonekana kwamba Kigweno kina asilimia kubwa ya msamiati ambao haupo kwenye lahaja nyingine za Kichaga. Hali hii inaonesha kwamba-msamiati mwingi uliazimwa kutoka lugha ya Chasu na mwingine kutoka lugha jirani kama vile Kikuyu, Kikamba na lugha nyingine zisizo za Kibantu.

### Historia Fupi Kuhusu Jamii ya Wagweno

Kimambo (1965) anaeleza kwamba Wagweno walifika Ugweno kutokea milima ya Taita na walifika eneo la Ugweno kabla ya Wasu. Maelezo haya yanaonesha kwamba lugha ya Kigweno imetoka Kenya hususani maeneo ya Taita. Katika utafiti uliofanywa na Kimambo kati ya–Julai 1965 na Juni 1966 anaeleza kwamba hadi kufikia karne ya 18 lugha ya Kigweno ilikuwa inazungumzwa katika eneo lote la milima ya Pare Kaskazini yaani Ugweno na Usangi. Chasu kilikuwa kinazungumzwa Pare ya Kusini. Ni katika kipindi hiki ambapo Wasu kutoka milima ya Pare ya Kusini walihamia eneo la Usangi lililopo Pare ya Kaskazini na hivyo lugha ya Kigweno na Chasu zikaanza kuchangamana (taz. O'Barr, 1973). Katika simulizi inayohusu namna jamii ya Wagweno walihama kutoka Taveta hadi Ugweno, Philipson (2000) anaeleza Wagweno walikuwa wanaishi maeneo ya Taveta karibu na Wakamba.

Shughuli kubwa ya Wagweno ilikuwa ufugaji ingawa wakati mwingine walilima mazao ya vyakula karibu na makazi yao. Wakamba nao shughuli yao kubwa ilikuwa uwindaji. Pia, nao walilima kwa kiasi kidogo kuzunguka makazi yao. Wakati kila jamii ikiendelea na shughuli zake za kujitafutia riziki, ulitokea mgogoro wa ardhi uliosababishwa na Wakamba kuchukua ardhi ya Wagweno. Pia, mgogoro ulichochewa na tabia ya Wakamba kuchukua mifugo ~~ya~~ wa Wagweno kwa nguvu ili kujipatia kitoweo hasa pale walipokosa. Jambo hili lilisababisha vita baina ya makabila haya mawili yaani Wagweno na Wakamba. Wagweno walipoona wanashindwa waliondoka kwenda Ugweno kupitia Kahe. Walipofika Kahe walikutana na Wachaga ambao nao waliwapiga. Wagweno wakaamua kuhama kuelekea milimani ambako ndiko Ugweno.[3]

Ingawa maelezo haya hayaoneshi ni kipindi gani hasa Wagweno walihama kutoka Taita kwenda Ugweno, utafiti wa Kimambo (1969) unaonesha kwamba Wagweno walihamia Ugweno muda mrefu zaidi kabla ya karne ya 13 (taz. Mreta, 2000).

### Lugha ya Chasu

Chasu ni lugha inayozungumzwa na wasemaji wanaoishi katika safu za Milima ya Pare iliyoko Kaskazini Mashariki mwa Tanzania katika wilaya ya Same na Mwanga, mkoani Kilimanjaro. Guthrie (1967) ameiainisha lugha hii katika kundi G.22. Kama ilivyoelezwa na Kimambo (1969), kabla ya karne ya 18 Wasu walikuwa wakiishi maeneo ya Pare ya Kusini na mwanzoni mwa karne ya 18 ndipo walipoanza kuhamia Pare ya Kaskazini. Kuhama kwa Wapare hao kutoka Pare ya Kusini kulichangia kuchangamana kwa lugha ya Kigweno na Chasu. Kuchangamana huku kwa lugha hizi kulisababisha lugha ya Kigweno kuathiriwa kwa kiasi kikubwa na lugha ya Chasu. Nurse (1977) anaeleza kuwa uhusiano kati ya msamiati wa lugha ya Chasu na Kigweno ni 49%. Anafafanua kwamba ~~k~~Kiwango hiki kinaonesha uhusiano wa lugha ambazo ni za kundi moja. Mreta (2000) anaeleza kwamba kuna uhusiano wa kihistoria kati ya Kigweno na Chasu wa takribani vizazi 10 vilivyopita.

### Kiunzi cha Nadharia

Uchanganuzi wa data za sura hii umeongozwa na Nadharia ya Mwachano-Makutano ya Lugha za Kibantu ambayo ilipendekezwa na Massamba (2007) inayoeleza msambao wa Wabantu waliofanya

[3] Maelezo haya ni masimulizi aliyoyapata Philippson kutoka kwa watoa taarifa wake wakati anafanya utafiti Ugweno (taz. Philippson, 2000).

mjongeo katika maeneo mbalimbali. Nadharia hii inafafanua kwamba wakati wa Mijongeo ya Wabantu kulikuwa na mwingiliano na mtagusano uliokuwa ukifanywa kati ya Wabantu wenyewe na kati ya Wabantu na jamiilugha nyingine. Jamiilugha zinazotengana katika harakati za kutafuta maisha, baadaye hukutana. Ili kuwezesha mawasiliano baina ya jamiilugha tofauti, baadhi ya jamii huacha baadhi ya vipengele vya lugha kama vile msamiati wa L1 na kutumia msamiati wa L2. Kadiri muda unavyopita, hizo lugha jirani zinaanza kufanana zaidi kuliko kutofautiana.

Nadharia hii imeongozwa na nadhariatete ambayo Massamba (2007) ameiita Nadhariatete ya Udugu na Udugu wa Mbali (Hans, 2014). Kwa mujibu wa nadhariatete hii, lugha za jamiilugha mbili zenye uhusiano wa kimnasaba (ndugu) na zenye mawasiliano ya karibu zinaweza kuathiriana[4] zaidi kuliko lugha za jamiilugha ambazo hazina uhusiano wa kimnasaba au mawasiliano ya karibu (ndugu wa mbali). Kinachosisitizwa hapa ni kuwa ili lugha ziathiriane kimsamiati, ni lazima lugha hizo ziwe na sifa zote mbili za uhusiano wa kimnasaba na mawasiliano ya karibu kwa wanajamiilugha wake.

Nadharia tete ya Ndugu na Ndugu wa Mbali inafafanua kwamba lugha za Kibantu ambazo zinapakana, zina uwezo mkubwa wa kufanana zaidi kuliko lugha za kundi hilohilo ambazo ziko mbali. Hivyo, Nadhariatete ya Ndugu na Ndugu wa Mbali imetumika katika kuchanganua data zinazoonesha uhusiano baina ya lugha tatu zilizofanyiwa utafiti ambazo ni: Kikamba, Kingweno na Chasu.

**Methodolojia**

Katika sura hii tumetumia mbinu linganishi ambayo hutumiwa na wanaisimu kujaribu kulinganisha lugha mbalimbali kubaini iwapo lugha hizo zinatoka katika fuko moja au zinatokana na mafuko ya lugha tofautitofauti. Katika kutumia mbinu linganishi, tumechunguza msamiati wa msingi wa lahaja mbili za Kikamba kutoka nchini Kenya na lugha mbili za Chasu na Kigweno kutoka nchini Tanzania. Lahaja ya Kikamba tuliyoiteua ni ile inayozungumzwa katika eneo la Mwingi na viunga vyake (kuanzia sasa LAKIMWI) ambayo inadhihirisha tofauti kubwa kifonolojia na kileksika ikilinganishwa na lahaja nyingine za Kikamba. LAKIMWI ina sauti tatu tofauti ambazo hazipo katika lahaja nyingine za Kikamba. Sauti hizi zimewafanya watafiti kama vile Mutiga (2002) kudai kwamba huenda lahaja hii imekopa kutoka lugha jirani kama vile Kitharaka na Kimeru au huenda ni sauti asilia za Kikamba ambazo lahaja nyingine za Kikamba zilipoteza. Madai haya yametuchochea kulinganisha lahaja hii na lugha za Kibantu zilizo mbali nayo ili kubaini iwapo sauti hizi zipo katika lugha za Kibantu kama vile Kigweno na Chasu. Sauti katika LAKIMWI ambazo hazipo katika lahaja nyingine za Kikamba ni kama inavyooneshwa katika Jedwali Na. 1 lifuatalo:

1. Kubadilishana msamiati.

Vol. 1 No. 1 (2023): ISSN (Online): 2958-4914
DOI: https://doi.org/10.58721/jkal.v1i1.96


**Jedwali Na. 1: Sauti katika LAKIMWI ambazo Hazipo katika Lahaja Nyingine za Kikamba**

| Na. | Sauti za Kifonolojia | Sauti katika Maneno ya LAKIMWI | Sauti za Maneno katika Lahaja ya Kimaandishi | Tafsiri kwa Kiswahili |
|---|---|---|---|---|
| 1. | /ɣ / (gh) | Ĩghoo | Ĩyoo | Jana |
| 2. | | Ûghûû | ûû | Chungu |
| 3. | | Ghĩanga | Yanga | Mhogo |
| 4. | /ʦ/ (tʰa) | ʦaa | Saa | Saa |
| 5. | | ûʦûû | Ûsûû | Uji |
| 6. | | kûʦemba | Kûsemba | Kukimbia |
| 7. | /r/ (r) | Kĩromo | Kĩlomo | Mdomo |

**Chanzo:** Data za Uwandani, 2018

Jedwali Na. 1 linaonesha kwamba sauti (gh) na /r/ zipo katika lugha ya Kigweno na Chasu. Aidha, data iliyotumiwa katika makala haya ilikusanywa uwandani kupitia orodha ya msamiati wa msingi waliopewa wazungumzaji wa Kikamba (wazungumzaji wa lahaja mbili tofauti), Kigweno na Chasu. Katika lugha ya Chasu data ilikusanywa eneo la Pare ya Kaskazini (chasu 1) na pare Kusini (chasu 2). Msamiati huo uliandikwa kwa lugha ya Kiswahili. Isitoshe, data hii imetajirishwa na uzoefu wa waandishi kama wazungumzaji wazawa wa lugha zinazojadiliwa. Pia, kulifanyika mahojiano na watumiaji wa lugha zote tatu. Mahojiano hayo yalifanyika ana kwa ana, kwa kutumia mawasiliano ya simu na mitandao ya kijamii kama vile whatsapp na baruapepe. Jumla ya maneno tisini (90) ya msamiati wa msingi yalikusanywa katika makundi matatu yaani msamiati wa viungo vya mwili, msamiati wa mazingira asili na msamiati wa matendo ya kila siku. Uchanganuzi wa data ulifanywa kiulinganishi na kuelezwa kitaamuli.

**Dhana ya Msamiati wa Msingi**

Massamba (2017) anaeleza kwamba msamiati wa msingi ni ule unaohusu vitu vilivyo vya kawaida katika mazingira ya wasemaji wa lugha zinazohusika, vitu vilivyo vya asili katika mazingira hayo, majina ya sehemu za mwili na shughuli za kila siku za jamii zinazohusika. Miongoni mwa sifa za msamiati wa msingi ni kwamba msamiati huo huhimili vishindo vya mabadiliko. Huwa ni imara sana na unatofautiana kwa kiasi kikubwa na msamiati utumikao katika mazingira mengine. Sehemu inayofuata inawasilisha data zilizotumika katika utafiti huu.

**Uchanganuzi wa Ulinganifu na Utofauti baina ya Lugha ya Kikamba, Kigweno, Chasu na Kiswahili**

Katika sehemu hii, tunalinganisha na kutofautisha msamati wa lugha zilizofanyiwa utafiti kama inavyoonekana katika Jedwali Na. 2 hapa chini.

**Jedwali 2: Msamiati wa Viungo vya Mwili**

| Na. | KIKAMBA 1[5] | KIKAMBA 2[6] | KIGWENO | CHASU[7] 1 | CHASU[8]2 | KISWAHILI |
|---|---|---|---|---|---|---|
| 1. | Nzwĩĩ | nzwĩĩ | Njui | nywii | nywii | nywele |
| 2. | mûtwe/kyongo | mûtwe/kĩongo | mrwe, mirwe | mtwi | mtwi | Kichwa, |
| 3. | ghitho, metho | Itho/metho | ritho, mitho | iritho | idhitho | jicho, macho |
| 4. | kûtû, matû | kûtû, matû | kurwi, marwi | ithikio | isikio | sikio, masikio |
| 5. | ûthyû, maûthyû | ûthyû, maûthyû | kyamu | bhusho | vusho | uso, nyuso |
| 6. | Ĩnyûû | ĩnyûû | mbua | pua | m'pua | pua |
| 7. | kĩromo, iromo | kĩlomo,ilomo | mumu | momo | momo | mdomo |
| 8. | kanywa | kanywa | mumu | momo | momo | kinywa |
| 9. | ĩtau, matau | ĩtau, matau | ndumbu | itumbu | itumbu | Shavu,mashavu |
| 10. | ĩgheo, magheo | yeyo, maeyo | ighegho, maghegho | ijegho | ijegho | Jino, meno |
| 11. | king'ethwa | king'ethwa | Teru | kireju | kirebu | kidevu |
| 12. | ngingo | ngingo | dhingo | thingo | thingo | shingo |
| 13. | kĩtuo, ituo | kĩtuo, ituo | ikotho, makotho | kituro | kituro | bega, mabega |
| 14. | kwoko, moko | kw'oko, moko | kubhoko, mabhoko | mkono | mkono | mkono, mikono |
| 15. | kyaa, syaa/nzaa | kyaa, syaa | mnyu, minyu | kichaa | kichaa | kidole, vidole |
| 16. | ngunyû | mbwaa | njwala | ngombe | kombe | kucha |
| 17. | Ĩvu | ĩvu | ndenyi | ndenyi | ndeni | tumbo |
| 18. | mwiyovo, ngunguo | kĩnyunyu | Kití | kikwidi | kivaju | kiuno |
| 19. | mûtambĩ, mĩtambĩ | Ĩtako, matako | ubhaha | kigha | kigha | paja, mapaja |
| 20. | lĩu,malu | Ĩlu, malu | | ikunguro | ikunguro | goti, magoti |

[5] Kikamba 1 ni lahaja ya Kikamba inayozungumzwa nchini Kenya, Kaskazini mwa kaunti ya Kitui eneo la Mwingi na viunga vyake. Ni lahaja inayojibainisha kwa kuwa na sauti tatu ambazo hazipo katika lahaja nyingine za Kikamba ila sauti mbili kati yazo zipo katika Kigweno na Chasu, lugha za Tanzania.

[6] Kikamba 2 ni lahaja ya Kikamba inayochukuliwa kuwa rasmi au sanifu na inayotumiwa kwa maandishi, matangazo na kufundishwa wale wanaotaka kujifunza Kikamba kama lugha ya kigeni.

[7] Chasu kinachozungumzwa maeneo ya Pare Kaskazini.

[8] Chasu kinachozungumzwa maeneo ya Pare Kusini.

| | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|
| 21. | kûghûû, maghûû | kûû, maaû | kurende, marende | kughu | kughu | mguu, miguu |
| 22. | ûnyayo, nyaayo | ûnyaaĩ | tubha | ibhato | ivato | wayo, nyayo |
| 23 | kĩtainyo, itainyo | kĩtiinyo | Tutu | tutunya | tutunya | kisigino, visigino |
| 24. | ĩtako, matako | kĩtimba, itimba | mbwecha | itako | nghunga | makalio |
| 25. | mwongo, miongo | mwongo, miongo | mghongo, mighongo | mghongo | mghongo | Mgongo, xmigongo |
| 26. | nondo | nondo | ibhele | ibhee | itombo | ziwa/titi |
| 27. | Ûĩme | ûĩme | ulimi | lumi | lumi | ulimi |
| 28. | Ĩkoti | ikoti | ighoti | ighoshi | kigoshi | kisogo |
| 29. | ngove | ngove | mughoi | ngohe | ngohe | kope |
| 30. | kĩthûi | kĩthûi | mbafu | mbafu | m'pafu | kifua |

**Chanzo:** Data za Uwandani, 2018

Journal of Kiswahili and Other African Languages
Vol. 1 No. 1 (2023): ISSN (Online): 2958-4914
DOI: https://doi.org/10.58721/jkal.v1i1.96


**Jedwali Na. 3: Mazingira ya Asili**

| Na | KIKAMBA 1 | KIKAMBA 2 | KIGWENO | CHASU 1 | CHASU 2 | KISWAHILI |
|---|---|---|---|---|---|---|
| 1. | ghûsĩ, mbûsĩ | Ûsĩ, mbusĩ | mfo, mifo | kyanda, vyanda | ndiva | mto, mito |
| 2. | Kĩĩma, syĩĩma | Kĩĩma, iĩĩma | mlima, milima | Mgongo | mgongo | mlima, milima |
| 3. | Mûtĩ, mĩtĩ | Mûtĩ, mĩtĩ | mri, miri | Mti | mti | mti, miti |
| 4. | Nyeki | Nyeki | Mara | Mani | mani | nyasi |
| 5. | Nyamû/nzoka | Nzoka | Njoka | Nyoka | nyoka | nyoka |
| 6. | mûthanga | Mûthanga | Mthangalala | mthangalale | mshangag a | mchanga |
| 7. | ndaka | Ndaka | Teri | Mthau | mthahu | udongo |
| 8. | Ĩvia, mavia | Ĩvia, mavia | ighwe, maghwe | Ibwe | ibwe | jiwe, mawe |
| 9. | ghĩiya | Ĩiya | Iribha | -idibha | idibha** | ziwa |
| 10. | mûûnda | Mûûnda | Ishamba | Shamba | konde, mghunda | shamba |
| 11. | kyanda | Kyanda | boto, maboto | Kyanda | kiindi | Bonde, mabonde |
| 12. | Kitheka, itheka, mûtitû | Kitheka, itheka | ithaka, mathaka | Mshitu | mshitu | msitu, misitu |
| 13. | Sua | Sua | Mbari | Idhubha | idhubha | jua |
| 14. | Mwei | Mwei | Mwiri | Mweji | mweji | mwezi |
| 15. | Ndeta | Ndata | Ndondo | Nyota | n'don'do | nyota |
| 16. | Ĩtu, matu | Ĩtu, matu | ilwi, mailwi | Ijumvi | ijumbi, majumbi | wingu, mawingu |
| 17. | nyomba | Nyumba | Nyumba | Nyumba | nyumba | nyumba |
| 18. | Nzĩa | Nzĩa | Njia | Dhia | dhia | njia |
| 19.. | Kûvyûva/ûvyûv u | Kûvyûva/ûvyû vu | Ndughuri | Ndughuri | kiruke, ndughuri | joto |
| 20. | Manzĩ/kĩw'û | Manzĩ/kĩw'û | Mringa | Madhi | madhi, m'pombe | maji |
| 21. | mbevo | Mbevo | Mbeho | Mbeho | m'peho | baridi |
| 22. | nzakame | Nthakame | Dhakame | Thakame | thakame | damu |
| 23. | Syuki | Ĩsyuki | Mti | Mushi | moshi | moshi |
| 24. | mwaki | Mwaki | Moro | Moto | moto | moto |
| 25. | Mûu | Mûu | Ifu | ibhu, maibhu | ivu | jivu/majivu |
| 26. | Ĩkaa, makaa | Ĩkaa, makaa | ikaa, makaa | Mkaa | mkaa | mkaa/makaa |
| 27. | mûndû, andû | mûndû, andû | mndu, bhandu | mndu, vandu | mntu | mtu, watu |
| 28. | ng'ombe | Ng'ombe | ng'umbe | ng'ombe | ng'ombe | ng'ombe |

| | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|
| 29. | Ĩkitĩ, ikurû | Ngitĩ | Kite | Iguro | iguro | mbwa |
| 30. | Ûkûngi/nzeve | Nzeve | Mkuta | Ngungu | n'kungu | upepo |

**Chanzo:** Data za Uwandani, 2018

**Jedwali Na. 4: Matendo ya Kila Siku**

| Na. | KIKAMBA 1 | KIKAMBA 2 | KIGWENO | CHASU 1 | CHASU 2 | KISWAHILI |
|---|---|---|---|---|---|---|
| 1. | kûtheka | Kûtheka | isheka | Kutheka | kutheka | kucheka |
| 2. | kûghĩa | Kûĩa | ifugha | Kuiya | kuiya | kulia |
| 3. | kûnywa | Kûnywa | inywa | Kunywa | kunywa | kunywa |
| 4. | Kûtembea/kûthi | Kûtembea/kûthi | itembea | Kubhata | kuvata | kutembea |
| 5. | kûsyaa | Kûsyaa | ighira | Kumogha | kumogha | kuzaa |
| 6. | Kûkw'a | Kûkw'a | Ifwa | Kufwa | kufwa | kufa |
| 7. | kûgha | Kûya | Iya | Kula | kula | kula |
| 8. | kûkoma | Kûkoma | Ilaa | Kushinjia | kushinjia | kulala |
| 9. | Kûamûka/kûkĩla | Kûamûka/kûkĩla | ibhukia | Kuvuka | kuvuka | kuamka |
| 10. | kûkooa | Kûkooa | iokola | Kukoha | kukoha | kukohoa |
| 11. | Kûongea | Kûongea | Irera | kuteta/kugaya | kugaya | kuongea |
| 12. | kûneena | Kûneena | Irera | Kugaya | kugaya | kuzungumza |
| 13. | kûthamba | Kûthamba | ithamba | Kukoja | kuhaka | kuoga |
| 14. | kwina | Kwina | iimba | Kuimba | kuimba | kuimba |
| 15. | kwĩnama | Kûĩnama | ikodeka | Kukodeka | kukodeka | kuinama |
| 16. | kûkĩla | Kûkĩla | iibhukia | Kuvukika | kuimuka | kuinuka |
| 17. | kwonga | Kwonga | ihonga | Kuamwa | kuamwa | kunyonya |
| 18. | kwithukĩĩsya | kwithukĩĩsya | iirania | Kusikija | kuthikija | kusikiliza |
| 19. | kwona | Kwona | ibhona | Kuvona | kuvona | kuona |
| 20. | kwombosya | kwombosya | ichunga | Kushinjiya | kuchunda | kusinzia |
| 21. | kwongola | Kûthaitha | ibembeletha | Kusemberej a | kuthemereja | kubembeleza |
| 22. | kumaa | Kumaa | iumagha | Kukwedhua | kupipie | kukojoa |
| 23. | kûmĩa | Kûmĩa | Inya | Kunya | kupipie | kunya |
| 24. | Kûng'ea | Kûya | Iibha | Kuiva | kuiva | kuiba/kudokoa |
| 25. | kûkania | Kûkania | ikanya | Kukanya | kukanya/kuchunda | kuonya/kataza |
| 26 | kûvoya | Kûvoya | ilomba | Kuomba | kutanja | Kuomba |
| 27. | kûthaûka | Kûthaûka | ichetha | Kucheza | kushenjigha | Kucheza |
| 28. | Kûthoosya/kûta | Kûthoosya | ikumba | Kutagha | kutaghija | Kuuza |
| 29. | Kûghûa/kuthoa | Kûûa | ighua | kudhora | kuzora | Kununua |
| 30. | kûua | Kûua | Ikora | Kurugha | kudika/kurugha | Kupika |

**Chanzo:** Data za Uwandani, 2018

**Matokeo na Mjadala**

Sehemu hii inawasilisha matokeo na mjadala wa data zilizotumika katika utafiti huu. Matokeo ya mjadala huu yamejikita katika vipengele viwili ambavyo ni kufanana na kutofautiana. Katika kutofautisha na kufananisha vipengele vilivyohusishwa ni msamiati na sauti. Sehemu inayofuata na inaonyesha kufanananana na kutofautiana kwa msamiati na sauti katika lugha ya Kikamba, Kigweno na Chasu.

**Kufanana kwa Msamiati na Sauti**
Tunapochunguza msamiati wa msingi baina ya lugha hizi, tunabaini kwamba kuna maneno mnasaba (cognate words) kama anavyoyaita Massamba (2007). Katika uchunguzi wa msamiati ilibainika kwamba kuna kufanana kwa msamiati wa lugha zote tatu zilizofanyiwa utafiti. Majedwali yanayofuata yanaonesha ufanano huo.

**Jedwali Na. 5. Kufanana kwa Msamiati wa Viungo vya Mwili**

| Na. | KIKAMBA 1 | KIKAMBA 2 | KIGWENO | CHASU 1 | CHASU 2 | KISWAHILI |
|---|---|---|---|---|---|---|
| 1. | nzwĩĩ | Nzwĩĩ | Njui | Nywii | nywii | Nywele |
| 2. | mûtwe, mĩtwe | mûtwe, mĩtwe | mrwe, mirwe | Mtwi | mtwi | Kichwa, vichwa |
| 3. | ghitho, metho | Itho, metho | ritho, mitho | Iritho | idhitho | jicho, macho |
| 4. | Kĩtuo, ituo | Kĩtuo, ituo | - | Kituro | kituro | bega, mabega |
| 5. | Ĩgheo, magheo | yeyo, maeyo | ighegho, maghegho | Ijegho | ijegho | jino, meno |
| 6. | ngingo | ngingo | dhingo | Thingo | thingo | Shingo |
| 7. | Kûghûû, maghûû | Kûû, maaû | - | Kughu | kughu | |
| 8. | Mwongo, miongo | Mwongo, miongo | mghongo | mghongo | mghongo | Mgongo |
| 9. | ûĩme | ûĩme | ulimi | Lumi | lumi | Ulimi |
| 10. | ngove | ngove | mghoi | Ngohe | ngohe | Kope |

**Chanzo:** Data za Uwandani, 2018

Data katika Jedwali Na. 5 zilifanyiwa ukokotoaji ili kupata asilimia ya msamiati wa viungo vya mwili unaofanana baina ya Kikamba, Kigweno na Chasu. Matokeo yanaonesha kwamba kati ya maneno 192, maneno 101 sawa na 52. % yanaonesha kufanana baina ya Kikamba 1, Kikamba 2, Kigweno, Chasu 1 na Chasu 2. Kielelezo hapa Na. 2 kinaonesha asilimia ya kufanana na kutofautiana kwa msamiati wa viungo vya mwili baina ya lugha hizi.


Aidha, ilibainika kwamba kati ya maneno 192 maneno 92 sawa na asilimia 48% yanatofatiana baina ya Kikamba 1, Kikamba 2, Kigweno, Chasu 1 na Chasu 2.

**Jedwali Na. 6: Kufanana na Kutofautiana kwa Msamiati wa Viungo vya Mwili baina ya Kikamba 1&2, Kigweno na Chasu 1&2**

| Msamiati Unaofanana | Msamiati Unaotofautiana | Jumla ya Msamiati |
|---|---|---|
| 101 | 92 | 192 |

Jedwali Na. 6 hapo juu linaonesha idadi ya msamiati wa viungo vya mwili unaofanana maneno 101/192 na msamiati unaotofautiana, maneno 92/192. Ukokotoaji wa asilimia umeoneshwa katika Kielelezo Na.2 katika ukurasa ufuatao.

**Kielelezo Na. 2: Kufanana na Kutofautiana kwa Msamiati wa Viungo vya Mwili baina ya Kikamba 1&2, Kigweno na Chasi 1&2**




**Chanzo:** Data za Uwandani, 2018

Katika sehemu inayofuata tunafafanua kiulinganishaji kufanana na kutofautiana kwa msamiati wa mazingira ya asili vaina ya lugha zilizofanyiwa utafiti yaani Kikamba 1&2, Kigweno na Chasi 1&2. Matokeo yameoneshwa kupitia kwa Jewali Na.7, Na. 8 na Kielelezo Na. 3 kama ifuatavyo:

**Jedwali Na. 7: Kufanana kwa Msamiati wa Mazingira ya Asili**

| Na. | KIKAMBA 1 | KIKAMBA 2 | KIGWENO | CHASU 1 | CHASU 2 | KISWAHILI |
|---|---|---|---|---|---|---|
| 1. | Mûtĩ, mĩtĩ | Mûtĩ, mĩtĩ | mri, miri | Mti | mti | mti, miti |
| 2. | Nyamû/nzoka | Nzoka | njoka | Nyoka | nyoka | Nyoka |
| 3. | Mûthanga | Mûthanga | mthangalala | mthangalale | mshangaga | Mchanga |
| 4. | Kitheka, itheka, Mûtitû | Kitheka, itheka | ithaka, mathaka | Mshitu | mshitu | Msitu |
| 5. | Mwei | Mwei | mwiri | Mweji | mweji | Mwezi |
| 6. | Nyomba | Nyumba | nyumba | Nyumba | nyumba | Nyumba |
| 7. | Nzĩa | Nzĩa | njia | Dhia | dhia | Njia |
| 8. | Manzĩ/kĩw'û | Manzĩ/kĩw'û | mringa | Madhi | madhi | Maji |
| 9. | Mbevo | Mbevo | mbeho | Mbeho | m'peho | Baridi |
| 10. | ng'ombe | ng'ombe | ng'umbe | ng'ombe | ng'ombe | ng'ombe |
| 11. | mûndû, andû | mûndû, andû | mndu | mndu, vandu | mntu, vandu | |

**Chanzo:** Data za Uwandani, 2018

Kwa kurejelea Jedwali Na. 7, matokeo ya ulinganishaji yanaonesha kwamba jumla ya maneno 167 yaliyokusanywa, maneno 98 sawa na 59 % yanadhihirisha kufanana kwa msamiati wa mazingira ya asili baina ya Kikamba 1, Kikamba 2, Kigweno, Chasu 1 na Chasu 2. Vilevile, kati ya maneno 167 maneno 69 sawa na 41 % yanatofautiana baina ya Kikamba 1, Kikamba 2, Kigweno, Chasu 1 na Chasu 2.


**Jedwali Na. 8: Kufanana na Kutofautiana kwa Msamiati wa Mazingira ya Asili baina ya Kikamba 1&2, Kigweno na Chasu 1&2**

| Msamiati Unaofanana | Msamiati Unaotofautiana | Jumla ya Msamiati |
|---|---|---|
| **98** | **69** | **167** |

**Chanzo:** Data za Uwandani, 2018

Kwa kurejelea Jedwali Na. 8 hapo juu, maneno 98/167 kuhusu msamiati wa mazingira ya asili unafanana baina ya lugha tatu na lahaja zake zilizochunguzwa. Pia, matokeo yanaonesha kwamba maneno 69/167 yanatofautiana. Ukokotoaji wa asilimia unaoneshwa katika Kielelezo Na. 3 hapa chini.

**Kielelezo Na. 3: Kufanana na Kutofautiana kwa Msamiati wa Mazingira ya Asili baina ya Kikamba 1&2, Kigweno na Chasi 1&2**




**Chanzo:** Data za Uwandani, 2018

Aidha, makala hii imefafanua kiulinganishi msamiati wa matendo ya kila siku na kuonesha kiwango cha ulinganifu na kutofautiana baina ya lugha zilizochunguzwa. Matokeo yameoneshwa katika Jedwali Na.9, Na.10 na Kielelezo Na.4. kama ifuatavyo:

**Jedwali Na. 9: Kufanana kwa Msamiati wa Matendo ya Kila Siku**

| Na. | KIKAMBA 1 | KIKAMBA 2 | KIGWENO | CHASU 1 | CHASU 2 | KISWAHILI |
|---|---|---|---|---|---|---|
| 1. | Kûtheka | Kûtheka | isheka | kûtheka | kûtheka | Kucheka |
| 2. | Kûghĩa | Kûĩya | ifugha | Kuiya | kuiya | Kulia |
| 3. | Kûnywa | Kûnywa | inywa | kunywa | kunywa | Kunywa |
| 4. | Kûtembea/kûthi | Kûtembea/kûthi | itembea | kubhata | kuvata | Kutembea |
| 5. | Kûkooa | kûkooa | iokola | kukoha | kukoha | Kukohoa |
| 6. | Kwona | kwona | ibhona | kuvona | kuvona | Kuona |
| 7. | Kûkania | kûkania | ikanya | kukanya | kukanya | Kuonya |
| 8. | Kûghûa/kuthoa | Kûûa | ighua | kudhora | kuzora | Kununua |
| 9. | Kûthamba | kûthamba | ithamba | kukoja | kuhaka | Kuoga |
| 10. | Kwonga | kwonga | ihonga | kuamwa | kuamwa | Kunyonya |

**Chanzo:** Data za Uwandani, 2018

**Journal of Kiswahili and Other African Languages**
Vol. 1 No. 1 (2023): ISSN (Online): 2958-4914
DOI: https://doi.org/10.58721/jkal.v1i1.96


Katika Jedwali Na. 10, matokeo ya ulinganishaji yanaonesha kwamba jumla ya maneno 130 yaliyokusanywa, maneno 85 sawa na 65 % yanadhihirisha kufanana kwa msamiati wa mazingira ya asili baina ya Kikamba 1, Kikamba 2, Kigweno, Chasu 1 na Chasu 2. Vilevile, kati ya maneno 130 maneno 45 sawa na 35 % yanatofautiana baina ya Kikamba 1, Kikamba 2, Kigweno, Chasu 1 na Chasu 2.


**Jedwali Na 10: Kufanana na Kutofautiana kwa Msamiati wa Matendo ya Kila Siku baina ya Kikamba 1&2, Kigweno na Chasu 1&2**

| Msamiati Unaofanana | Msamiati Unaotofautiana | Jumla ya Msamiati |
|---|---|---|
| 85 | 45 | 130 |

**Chanzo:** Data za Uwandani, 2018

Uchanganuzi kiulinganishi unaonesha kwamba maneno 85/130 ya msamiati wa matendo ya kila siku unafanana na maneno 45/130 ya msamiati huo yanatofautiana. Hivyo, Kikamba 1&2, Kigweno na Chasu 1&2 zinafanana kwa 65 % na kutofautiana kwa 35 % kuhusu msamiati wa matendo ya kila siku ambayo ni shughuli za msingi za binadamu. Kielelezo Na. 4 kinaonesha ukokotoaji wa asilimia.

**Kielelezo Na. 4: Kufanana na Kutofautiana kwa Msamiati wa Matendo ya Kila Siku baina ya Kikamba 1&2, Kigweno na Chasu 1&2**




**Chanzo:** Data za Uwandani, 2018

**Matokeo**

Tunapochunguza majedwali hapo juu kuhusu msamiati wa msingi baina ya lugha za Kikamba, Kigweno na Chasu, kuna maneno yanayofanana kama vile 'nyomba/nyumba', 'ng'ombe', 'kutheka',

'kuiya', 'kunywa', 'kutembea', 'kukania/kukanya (taz. jedwali 5, 6 na 7). Hata pale ambapo maneno hayafanani kwa kila silabi, kuna maumbo yanayofanana kuonesha kwamba lugha hizi zinatokana na fuko moja lakini kutokana na kutengana kwa muda mrefu, sauti zikabadilika kwa kuathiriwa na lugha jirani na kutokea mifanyiko ya kifonolojia. Kwa mfano, 'nzoka', 'njoka' na 'nyoka' (taz. Jedwali…). Pia, 'nzia', 'njia', 'dhia' (njia). Halikadhalika, lugha zote zinaonesha kufanana kwa neno 'mutwe' (kichwa). Hata pale Kigweno kinapotumia 'murwe' ni tofauti ya sauti moja /r/ na /t/. Data zilizowasilishwa katika majedwali hapo juu zinaonesha kufanana kwa msamiati katika lugha zote tatu zilizochunguzwa. Vile vile, tulibaini kwamba ufanano wa msamiati unabainika zaidi katika matamshi kuliko katika maandishi. Kwa mfano, maneno kama vile nzwĩĩ, njui, nywii (nywele), nzoka, njoka, nyoka (nyoka) kûkania, ikanya, kukanya (kukanya). Tukichunguza maneno haya inaonekana dhahiri kwamba yanafanana kwa kiasi fulani wakati wa kuyatamka kuliko yanavyoonekana kimaandishi.

Aidha, tulibaini kwamba kuna maneno ambayo yanatumia mzizi uleule, tofauti kati ya lugha moja na nyingine inakuwa katika viambishi awali vilivyopachikwa katika mzizi wa neno. Kwa mfano, neno kama mûndû-andû, m**ndu**- bha**ndu**, m**ntu**-va**ndu** (mtu) mw**ongo**, miongo, mgh**ongo**, migh**ongo** (mgongo, migongo). Ufanano wa msamiati ulioonyeshwa katika Jedwali Na. 5, 6 na 7 unashabibiana na maelezo ya Massamba (2007) katika Nadharia ya Ndugu na Ndugu wa Mbali kwamba ikiwa lugha ni ndugu (yaani zinatoka katika fuko moja) lugha hizo hufanana kimsamiati.

**Kutofautiana kwa Lugha Zilizochunguzwa**
Kwa kurejelea msamiati wa msingi katika Jedwali Na. 2, 3 na 4 kuna kutofautiana kwa baadhi ya sauti kama inavyodhihirika katika Jedwali Na. 11 hapa chini.

**Jedwali Na. 11: Tofauti za Sauti baina ya Kikamba, Kigweno na Chasu**

| Na. | KIKAMBA 1 | KIKAMBA 2 | KIGWENO | CHASU 1 | CHASU 2 | KISWAHILI |
|---|---|---|---|---|---|---|
| 1. | **gh**itho, m**e**tho | Itho, m**e**tho | **r**itho, m**i**tho | **Ir**itho | **idh**itho | Jicho, macho |
| 2. | **ng**ingo | **ng**ingo | **dh**ingo | **Th**ingo | **th**ingo | Shingo |
| 3. | Mbe**v**o | mbe**v**o | mbe**h**o | Mbe**h**o | m'**pe**h**o** | Baridi |
| 4. | **Kw**ona | **Kw**ona | **ibh**ona | **Kuv**ona | **kuv**ona | Kuona |

**Chanzo:** Data za Uwandani, 2018

Huenda mabadiliko haya yametokana na kuathiriana baina ya lugha moja na nyingine au kutokana na lugha moja kutokuwa na sauti zinazotumika katika lugha nyingine. Kikamba kina irabu saba ilhali Kigweno na Chasu zina irabu tano. Tofauti nyingine inajitokeza katika viambishi. Kwa kurejelea msamiati wa msingi kama unavyooneshwa katika majedwali 2,3 na 4 tunabainisha kwamba lugha za Kikamba na Chasu zinatumia viambishi awali vinavyokaribiana tofauti na viambishi awali vya Kigweno kama inavyooneshwa katika Jedwali Na. 12:

**Jedwali Na. 12: Kufanana kwa Viambishi Awali Kati ya Kikamba na Chasu Tofauti na Kigweno**

| Na. | Kikamba 1 | Kikamba 2 | Kigweno | Chasu1 | Chasu 2 | Kiswahili |
|---|---|---|---|---|---|---|
| 1. | **Kû**kooa | **Kû**kooa | **i**okola | **Ku**koha | **ku**koha | **Ku**kohoa |
| 2. | **Kû**kania | **Kû**kania | **i**kanya | **ku**kanya | **ku**kanya | Kukanya |
| 3. | **Kû**nywa | **Kû**nywa | **i**nywa | **Ku**nywa | **ku**nywa | Kunywa |
| 4. | **Kû**theka | **Kû**theka | **is**heka | **Ku**theka | **ku**theka | Kucheka |
| 5. | **Kû**ghĩya | **kû**iya | **ifugha** | **Ku**iya | **ku**iya | Kulia |

**Chanzo:** Data za Uwandani 2018

Kwa kurejelea data katika Jedwali Na. 12, tubainisha kwamba Kikamba na Chasu zinatumia kiambishi 'ku' ya kitenzi kisoukomo tofauti na Kigweno ambacho kinatumia 'i'. Tungetarajia lugha za Chasu na Kigweno zifanane lakini hali inakuwa tofauti ambapo Kikamba kinachozungumzwa mbali hususan lahaja ya Kikamba ya Mwingi inafanana na Chasu katika matumizi ya kiambishi 'ku' kuliko Kigweno kilicho karibu. Hali hii ni kinyume cha Nadhariatete ya Ndugu na Ndugu wa Mbali.

Aidha, ilibainika kwamba baadhi ya msamiati wa lugha ya Kigweno ambao ni tofauti kabisa na ule wa Kikamba na Chasu umechukuliwa kutoka lugha ya Kikahe ambayo ni lahaja mojawapo ya lugha ya Kichaga. Kama ilivyoelezwa hapo awali Wagweno walihama kutoka Taveta kwenda Ugweno lakini kabla ya kufika Ugweno walikaa kwa muda maeneo ya Kahe. Jedwali la 13 linaonesha msamiati wa Kigweno unaotofautiana na Kikamba na Chasu.

**Jwedwali Na. 13: Maneno ya Kigweno Yaliyotofautiana na Kikamba na Chasu**

| Na. | Kikamba 1 | Kikamba 2 | Kigweno | Kikahe | Chasu1 | Chasu 2 | Kiswahili |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| 1. | manzĩ/kĩw'û | kĩw'û | mringa | mringa | Madhi | madhi | maji |
| 2. | ng'ombe | ng'ombe | ng'umbe | ng'umbe | ng'ombe | ng'ombe | ng'ombe |
| 3. | kûghĩya | kûĩya | ifugha | Fugha | Kuiya | kuiya | kulia |
| 4. | kûua | kûua | ikora | Kora | kurugha | Kudika/kurugha | kupika |

**Chanzo:** Data za Uwandani, 2018

Kama inavyoonekana katika Jedwali Na. 13 hapo juu, Wagweno walichukua baadhi ya msamiati kutoka lugha ya Kikahe na kuacha msamiati waliokuwa wanatumia katika lugha yao ili kurahisisha mawasiliano kati yao na Wakahe. Massamba (2007) anaeleza katika Nadharia ya Ndugu na Ndugu wa Mbali kwamba ili kuwezesha mawasiliano baina ya jamiilugha tofauti, baadhi ya jamii huacha baadhi ya vipengele vya lugha kama vile msamiati wa L1 na kutumia msamiati wa L2. Hii ndiyo sababu msamiati wa lugha ya Kigweno unatofautiana na lugha ya Kikamba na Chasu.

Vilevile, imebainika kwamba lahaja ya Kikamba ya Mwingi ambayo watafiti waliotangulia (Maundu, 1980; Mutiga, 2002; Mathooko, 2004, Ngesu, 2004) wanakubaliana kwamba ina sauti ambazo hazipo katika lugha ya Kikamba, sauti hizo zipo katika Kigweno na Chasu. Hali hii inakinzana na Nadhariatete ya Massamba kwamba lughajamii mbili ambazo zina mnasaba (yaani zinatokana na mame-lugha moja) na zipo katika mtangusano huathiriana zaidi kuliko lugha za aina hiyohiyo ambazo ziko mbali zaidi kimasafa. Lugha ambazo ziko mbali ndizo zinazojulikana kama ndugu wa mbali. Katika makala hii, lahaja ya Kikamba ya Mwingi ina uhusiano wa ndugu wa mbali na Kigweno

na Chasu. Hata hivyo, hali inayodhihirika kwa data tuzizokusanya ni kwamba kuna kufanana baina ya lahaja ya Kikamba ya Mwingi na Chasu hata kuliko jinsi Kigweno kinafanana na Chasu. Sauti za lahaja ya Kikamba ya Mwingi ambazo watafiti wanadai zimekopwa kutoka lugha jirani na kwamba si sauti za Kikamba zinafanana na sauti za Kigweno na Chasu kama inavyooneshwa katika Jedwali hapa chini:

**Jedwali Na. 14 Kufanana kwa Msamiati na Sauti Baina ya Lahaja ya Mwingi na wa Chasu na Kigweno**

| Na. | KIKAMBA 1 | CHASU 1 | CHASU 2 | KIGWENO | KISWAHILI |
|---|---|---|---|---|---|
| 1. | iku**r**û | Igu**r**o | Igu**r**o | kite | Mbwa |
| 2. | nzwĩĩ | nywĩĩ | Nywĩĩ | njui | Nywele |
| 3. | Ĩ**gh**eo, ma**gh**eo | ije**gh**o | ije**gh**o | **ighegh**o, ma**ghegh**o | Jino, meno |
| 4. | **Kûghû**û, maghûû | **kughu** | **Kughu** | kurende, marende | Mguu, miguu |
| 5. | Mûtĩ, mĩtĩ | Mti, miti | Mti, miti | Mri, miri | Mti, miti |
| 6. | Kû**ghûa**/kuthoa | kudhora | Kuzora | **ighua** | Kununua |
| 7. | **mwe**i | **mwe**ji | **Mwe**ji | mwiri | Mwezi |

**Chanzo:** Data za Uwandani, 2018

**Hitimisho**

Makala hii imeonesha kwamba kuna ulinganifu wa kiwango kikubwa, baina ya lugha za Kikamba, Kigweno na Chasu ingawa wazungumzaji wake wako katika nchi tofauti (Kikamba-Kenya, Kigweno na Chasu-Tanzania) na hawana utangamano wa kila siku. Matokeo yanaonesha kwamba kuna kufanana kwa msamiati wa viunngo vya mwili kwa 52 %, msamiati wa mazingira asili kwa 59% na msamiati wa matendo ya kila siku kwa 65 % baina ya lugha za Kikamba, Kigweno na Chasu. Kwa upande mwingine ilibainika kwamba kuna kutofautiana kwa msamiati wa viunngo vya mwili kwa 48 %, msamiati wa mazingira asili kwa 41 % na msamiati wa matendo ya kila siku kwa 35% baina ya lugha za Kikamba, Kigweno na Chasu. Msamiati mwingi kama ulivyooneshwa katika Jedwali Na. 5, 6 na 7 unashabihiana kwa sauti na panapotokea tofauti ya sauti hizo, inabainika sauti hizo zinatamkiwa mahali pamoja au zimetokana na kuathiriwa na lugha jirani na pia utengano wa muda mrefu. Hivyo, lugha za Kikamba, Kigweno na Chasu zina mnasaba wa karibu na msamiati wa msingi pamoja na mfumo wa sauti unadhihirisha hivyo. Aidha, wazungumzaji wa Kigweno na Chasu wanatangamana mara kwa mara nchini Tanzania na hivyo kama ilivyo Nadhariatete ya Ndugu na Ndugu wa Mbali kuna kufanana kwa msamiati kuliko lugha hizo zinavyofanana na Kikamba. Hata hivyo, makala haya yameonesha kwamba kinyume na inavyodaiwa na Nadhariatete kwamba Ndugu wa Mbali watatofautiana kwa kiasi kikubwa, lahaja ya Kikamba ya Mwingi inayozungumzwa mbali sana, Kaskazini mwa Kaunti ya Kitui inashabihiana kisauti na lugha ya Chasu nchini Tanzania tofauti na lahaja ya Kikamba ya kimaandishi. Tunapendekeza utafiti ufanywe ili kuchunguza kwa kina hali hii ya kiisimu yaani lahaja moja ya Kikamba 1 inayozunguzwa mbali sana inafanana na lugha ya Kigweno, Chasu 1 na Chasu 2 kwa kiasi kikubwa.

Vol. 1 No. 1 (2023): ISSN (Online): 2958-4914
DOI: https://doi.org/10.58721/jkal.v1i1.96


**Marejeo**

Guthrie, M. (1948). *The Classification of Bantu Languages*. Oxford: Gregg Press.

Heine, E. and Mohlig (1980). *Language and Dialects Atlas of Kenya*. (Vol. J). Berlin: Dietrich Reinevmer Verlag.

Mathooko, P.M. (2004). *An Intergated Perspective of Language Accomodation: A Case Study of Kitharaka and Kikamba.* Tasnifu ya Uzamivu, Chuo Kikuu cha Nairobi.

Massamba, D.P.B. (2017). Historia ya Kiswahili 50BK hadi 1500BK. Nairobi: Jomo Kenyata Foundation.

Massamba, D.P.B. (2007). Kiswahili Origins and Bantu Divergence-Covergence Theory. Dar es Salaam: Institute of Kiswahili Research.

Maundu, P. M. (1980). Sound Change and the Reconstruction of Kikamba Consonantal Sound in Natural Generative Phonology Framework. Tasnifu ya Umahiri, Chuo Kikuu cha Nairobi.

Mreta, A.Y. (2000). "The Nature and Effects of Chasu-Kigweno Contact. Katika Languages of Tanzania. Leiden: Research School CNWS, Leden University. Uk. 177-190.

Mulatya, M.K. (2013). Comprehension of Kikamba Proverbs: A Study of Standard Eight Pupils of the Kawethei Primary School, Kangundo District, Machakos County. Tasnifu ya Umahiri, Chuo Kikuu cha Nairobi.

Muthoka, G.M. (2017). Kikamba Language Shift and Endangerment in an Urban Upmarket Setting: A Sociolinguistic Analysis. Tasnifu ya Umahiri, Chuo Kikuu cha Kenyatta.

Mutiga, J.M. (2002). The Tone System of Kikamba: A Case Study of Mwingi Dialect. Tasnifu ya Uzamivu, Chuo Kikuu cha Nairobi.

Mutua, N.B. (2013). A Constraint-Based Analysis of Kikamba Nativized Loanwords. Tasnifu ya Umahiri (haijachapishwa), Chuo Kikuu cha Kenyatta University.

Ngesu, S.N.M. (2004). Usilimisho wa Maneno Mkopo katika Lahaja ya Kikamba ya Mwingi. Tasnifu ya Umahiri (haijachapishwa), Chuo Kikuu cha Nairobi.

Nurse, D & Philpson G. (1980). "The Bantu Languages of East Africa: A Lexicolstatistical Survey. Katika Languages of Tanzania. London. Oxford University Press uk. 26-67.

O'Barr, W.M. (1973). "The Pare of Tanzania" Katika Tradition and Identity in Changing Africa. New York. Harper & Row.

Philippson, G & Nurse D. (2000). Gweno, A Little-Known Language of Northern Tanzania. Katika Languages of Tanzania. Leiden: Research School CNWS, Leden Universiry, uk. 233-286.

Winter, J.C. (1980). International Classfication of Kilimanjaro Bantu Compared: Towards EastAfrican Dialectomentry Katika Dialectologies Etcomparatisme en Afrique Noire. Paris: SEAF, uk. 101-132.